



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA  
TEKNOLOJIA YA HABARI

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA



## TAARIFA KWA UMMA

### UFAFANUZI JUU YA BEI ZA HUDUMA ZA DATA NCHINI

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na. 12 ya mwaka 2003 kusimamia huduma za kielektroniki na posta na masafa ya mawasiliano katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

TCRA inapenda kutoa ufafanuzi wa bei za huduma za data kama ifuatavyo:-

Bei za huduma za mawasiliano ya simu zimegawanyika katika makundi mawili, ambayo ni bei za kawaida na bei za huduma ndani ya vifurushi. Bei za kawaida (nje ya vifurushi) ni bei wanazolipa watumiaji wa huduma za kupiga simu, kutuma jumbe fupi au matumizi ya data bila ya kujiunga na vifurushi. Aidha, huduma za vifurushi zinaambatana na masharti ya kikomo cha muda pamoja na matumizi mfano ni; vifurushi vya siku, wiki, mwezi, vya wanachuo, vya usiku, vya maeneo maalum, n.k. ambavyo huwa vinabadilika kutokana na uhitaji. Kwa lugha nyepesi, vifurushi ni sawa na “buffet”, ambapo mteja anaweza kula au kunywa chochote kilichopo kwenye “package” hiyo ndani ya muda maalum.

Vigezo mbalimbali vinavyotumika na watoa huduma katika kupanga bei za huduma za mawasiliano ikiwemo data ni pamoja na gharama za uwekezaji na uendeshaji, idadi ya watoa huduma na muundo wa soko, Sera, Sheria na Kanuni zinazosimamia sekta, ukubwa wa nchi na upatikanaji wa rasilimali wezeshi za mawasiliano.

Takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya 95% ya watumiaji wa huduma za mawasiliano wanapendelea kutumia huduma za vifurushi kwa kuwa zina punguzo kubwa, hivyo kuweka unafuu katika matumizi ya huduma za Mawasiliano. Endapo mtumiaji ataamua kutumia data bila kujiunga kifurushi atatozwa bei za kawaida. Aidha, suala la data kuisha haraka huchangiwa na sababu mbalimbali zikiwemo kuongezeka kwa kasi ya mtandao na uwezo wa Simu-Janja, kuongezeka kwa ubora wa picha na video ambazo huongeza ukubwa, kuwa na programu rununu (mobile apps) nyingi zinazojihisha mara kwa mara bila mtumiaji kujua.

TCRA ina utaratibu wa kufanya stadi za bei za huduma za mawasiliano ambapo stadi ya sasa inaonesha kuwa gharama halisi ya kuuza data hapa nchini ni kati ya TZS 2.03/Mb hadi TZS 9.35/Mb. TZS 2.03/Mb ni bei ambayo Mtoa Huduma anaweza kuuza Data na kurudisha gharama zake za uendeshaji; na TZS 9.35/Mb ni bei ambayo mtoa huduma anaweza kuuza data na kutoa huduma zenye ubora na kuwafikia wananchi wengi zaidi.

## **Utafiti na ulinganisho wa Unafuu wa Bei za Data**

Kwa mujibu wa tafiti mbalimbali za bei za huduma za data, nchi yetu kwa sasa ndiyo ina bei ya chini zaidi kwa Mb kwa nchi za Afrika Mashariki na SADC ambapo wastani wa gharama za data nchini ni takribani dola 0.75 za Kimarekani kwa Gb moja ya data sawa na shilingi za Kitanzania TZS 1,725 (sawa na TZS 1.68/Mb).

Aidha, barani Afrika, Tanzania ni miongoni mwa nchi 6 kati ya 52 zenye gharama nafuu za data. Matokeo ya tafiti hizo yanapatikana kupitia viunganishi vifuatavyo:-

- i. <https://techcabal.com/2021/09/13/ten-african-countries-with-the-cheapest-data-plans/>
- ii. <https://www.visualcapitalist.com/cost-of-mobile-data-worldwide/>
- iii. <https://www.cable.co.uk/mobiles/worldwide-data-pricing/>

## **Hali ya Bei za Data kwa sasa**

Kanuni ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Bei za Huduma) ya mwaka 2018 inamtaka mtoa huduma kuwasilisha bei zake TCRA kila robo mwaka. Bei zilizowasilishwa, kuidhinishwa na ambazo zinatumiwa hivi sasa ziko ndani ya wigo wa bei uliokubalika. Bei ya data kwa sasa inaanzia TZS 1.5/Mb hadi TZS 9.35/Mb.

## **Hitimisho**

Mamlaka ya Mawasiliano inaendelea kuwasimamia watoa huduma ili kuhakikisha kwamba Sheria na Kanuni za huduma za Mawasiliano zinafuatwa kwa maslahi mapana ya Nchi yetu.

**IMETOLEWA NA MKURUGENZI MKUU  
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

**TAREHE 9/05/2022**